USIMAMIZI WA MAJANGA (RISK MANAGEMENT)

YALIYOMO

- Lengo la Mada
- Utangulizi
- Maana ya Majanga
- Utambuzi wa Majanga
- Aina za Majanga
- Mikakati ya Udhibiti
- Wajibu wa Bodi na Menejimenti katika kusimamia Majananga
- Hitimisho

LENGO LA MADA

Lengo la mada hii ni kujadili namna ya kuandaa Mwongozo wa usimamizi wa majanga pamoja na kujadili namna ya kujikinga na majanga hayo kwa lengo kupunguza uwezekano wa kutokea kwa athari (majanga) chamani.

UTANGULIZI

Majanga ni nini?

Majanga

Majanga ni matukio yasiyotarajiwa ambayo yanaweza kutokea na kusababisha chama kishindwe kufika malengo yake. Athari yake ni kushuka kwa mapato na kusababisha hasara chamani.

UTAMBUZI WA MAJANGA

Ili kuweza kuyatambua majanga, ni muhimu kuwepo na kitabu cha usajili wa majanga ambacho kinaweza kuwa katika mfumo ufuatao. (Risk Register)

Kitabu cha Usajili wa Majanga (Risk Register)							
Na	Aina ya Janga	Maelezo ya Janga	Kiwango cha Kutokea	Kiwango cha madhara	Alama (Watani wa kiwango cha matokeo na madhara)	Mhusika wa Usimamizi	Namna ya Kuzuia Janga
1	Moto	kutokea kwa moto katika jengo la chama			5	JJ KMC	Bima
2					3	Safari	
3					2		
4					5		
5					3		
6					2		
7					1		

AINA ZA MAJANGA

Yafuatayo ni baadhi ya majanga yanaweza kuikumba chama.

A. Majanga ya Mikopo.

Vihatarishi vya mikopo ni hali ya uwezekano kwamba mkopaji hana nia au uwezo wa kulipa riba na mkopo (Principle) kwa mujibu wa mkataba au makubaliano ya ukopeshaji wa mikopo na hivyo kusababisha hasara za fedha kwa wakopeshaji.

Inaendelea……

B. Majanga ya Kiutendaji.

Majanaga ya kiutendaji ina maana vihatarishi vya kupata hasara iliyosababishwa na mapungufu ya udhibiti wa ndani, watumishi na mfumo wa taarifa ya teknolojia,

Inaendelea…….

C. MAJANAGA YA TEKNOLOJIA NA MAWASILIANO.

Chama kinavyoendelea kukua kinategemea sana teknolojia. Hata hivyo chama kinaweza kupata janga la kiteknolojia pale mfumo wa tehama unapoweza kudukuliwa ama kufanya matumizi yasiyo faa

Inaendelea…….

D. MAJANGA YA UKWASI

Mfululizo wa ukosefu wa ukwasi chamani unaweza kupelekea chama kuwa na upungufu wa fedha na kushindwa kutoa huduma zake kwa wanachama na hivyo kuwa na uwezekanowa kufirisika.

Inaendelea……

E. MAJANGA YA SOKO

Vihatarishi vya soko vinaweza kusababisha kupotea kwa mapato ya chama au mtaji vinavyotokana na mabadiliko ya viwango vya riba, ubadilishaji wa fedha za kigeni au bei ya bidhaa.

Maeneo sugu ya vyanzo vya vihatarishi vya soko ni kutokana na riba kwa sababu ya upungufu wa mikopo na vyanzo vya fedha, amana au deni.

Inaendelea……

F. MAJANGA YA UWEKEZAJI

Kutokana na shughuli za uwekezaji, chama kinakuwa na uwezekano wa kukumbana na vihatarishi vya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika sehemu isiyo kuwa na tija na kupata hasara. Chanzo cha vihatarishi vya uwekezaji ni hutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kisera na matakwa ya kisheria.

MIKAKATI YA UDHIBITI

Udhibiti wa majanga unapaswa kutazingatia matokeo ya janga husika kama ifuatavyo.

A. JANGA HATARISHI

- Kuepuka janga (Avoid) mfano kutojishughurisha na kazi husika yenye kuhatarisha raslimali za chama
- Hamisha janga (Transfer) mfano kukata bima,
- Zuia (mitigate) mfano kuweka vizima moto kwenye jengo (Fire extinguisher)
- kubali (Acceptance) (kuamuna kuishi na janga husika)

Inaendelea...

B. JANGA LA KAWAIDA

- Buni njia mbadala (Exploit). Kutumia janga husika kuwa sehemu ya fursa kwa kubuni njia mbalimbali zinazoleta matokeo chanya
- Shirikisha (Share). Mfano kuingia mkataba na mtu au taasisi kushiriki kwa pamoja katika biashara Fulani.
- Boresha (Enhance). Mfano kuboresha namna ya uendeshaji wa shughuli za chama
- Kubali (Acceptance)

WAJIBU WA BODI NA MENEJIMENTI KATIKA KUDHIBITI MAJANGA

WAJIBU WA BODI KATIKA KUDHIBITI VIHATARISHI

Wajibu maalum wa wajumbe wa Bodi katika kusimamia vihatarishi vya kimkakati ni pamoja na:-

- Kuanzisha malengo ya Jumla ya Chama, malengo maalum ya kimkakati na msingi wa maono ya chama unaoelezea sababu za uwepo wa chama na kuhakikisha hayo yote yanawasilishwa, yanazingatiwa kikamilifu na kutekelezwa katika ngazi zote za chama kwa ufanisi.
- Kuhakikisha utekelezaji wa mwongozo wa usimamizi wa majanga unaendana na mpango mkakati wa chama
- Kuhakikisha kwamba mfumo mzima wa utambuzi na udhibiti wa vihatarishi vya kimkakati unasimamiwa katika namna ambayo itakuwa imara na inaendana na mpango mkakati wa maendeleo ya biashara.

Inaendelea.....

Wajibu wa ngazi ya juu ya uongozi katika mwongozo wa usimamizi wa majanga ya kimkakati wa chama ni kama ifutavyo;

- Kuanzisha na kutekeleza mfumo wa usimamizi na udhibiti wa vihatarishi vya kimkakati kwa kuzingatia vigezo na viwango vilivyowekwa na Bodi.
- Kusaidia Bodi katika kutengeneza mikakati ya maendeleo ili kukidhi malengo mahususi ya kimkakati na malengo ya jumla ya chama.
- Kuanzisha mipango mikakati ya utekelezaji ya chama katika kuendeleza shughuli za chama na mipango ya biashara

Inaendelea…….

- Kuhakikisha mpango mkakati ulioidhinishwa na bodi unatekelezwa kwa ufasaha
- Kutekeleza kwa uimara mfumo wa mapitio ya matokeo ya shughuli za chama
- Kuhakikisha kwamba mambo ya kimkakati na majanga makubwa yanayotokana na mabadiliko ya kimazingira au utekelezaji wa mpango mkakati wa chama vinaripotiwa kwa Bodi mara kwa mara kwa wakati.

HITIMISHO

Ni matumaini kuwa, kila chama kitaboresha mwongozo wa usimamizi wa majanga na kila mmoja kwa nafasi yake atahakikisha mwongozo unatekelezwa vyema ili kujiepusha na madhara yanayoweza kujitokeza Chamani

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA